



MAFUNZO YA JINSI YA KUTUMIA KIBABA MFS

Kibaba

Program ya Vicoba

Jarida la Mwezi

Kibaba, Programu ya ViCoBa

by Frank Mwasalukwa

Kibaba MFS ni nini?

Kibaba ni Program yenye uwezo wa kurahisisha kazi zinazofanywa na Vikundi ya Kuweka na Kukopa yaani ViCoBa, MFI na Upatu.

Ukiwa na Programu hii utahitaji Kompyuta au simu au Tableti ili uweze kuweka kumbukumbu mbalimbali za wanachama. Hii itasaidia Kikundi kuachana na utegemezi pekee wa Kadi, Vitabu vya hesabu na Excel (Spreadsheet).

Nini Programu hii inafanya

Kibaba MFS ni Program ilobuniwa ili kurahisisha kazi za kila siku za kutunza taarifa kwenye vikundi vya ViCoBa.

Program hii itakuwezesha kutunza taarifa za Wanachama na taarifa za

Fedha na michango yote ya kila siku iliwemo mikopo na Marejesho.

Programu hii ya ViCoBa ina uwezo wa kubadilisha sharia na Taratibu za kikundi husika cha ViCoBa na kuzifanya kuwa za kieletrini, mfano Riba ya mkopo, Kiwango cha kukopa cha **Mwanachama**, n.k. Lakini pia inaweza kusajili **Wanachama** wapya, Kusajili Hisa zao, kusajili mikopo na marejesho yake.

Pia Programu hii inatoa fursa kwa wanachama wote kuweza kuingia kwa kutumia simu zao janja, Tabili au Kompyuta popote walipo.

Programu inatumia Intaneti na Vifaa kama Simu, Tabiti au Kompyuta



Warsha ya Mafunzo ya Kibaba

Washiriki wa moja wapo ya Warsha ya mafunzo ya Kibaba katika Ukumbi wa YWCA – Dar Branch. Washiriki kutoka Vikundi mbalimbali vya ViCoBa vya Dar es Salaam.



Relax, Ni rahisi kutumia

Kibaba MFS ni rahisi sana kuitumia, Kila mmoja kwenye kikundi cha ViCoBa anaweza kutumia Program, Ipo kwa lugha iliyozoeleka ya Kiswahili na Lugha za ViCoBa

Kama utahitaji kujaribu kabla ya kuninia ingia hapa
<http://demo.kibaba.co.tz>

Features/Vipengele

by Lilian W. Mushi

Kibaba imeundwa kwa kuangalia mfumo mzima wa ViCoBa unavyofanya kazi, Kibaba imegawanyika katika sehemu kuu nne ambazo pia na zenyewe zina vipengele vidogo vidogo.

✚ Mipangilio ya Mfumo

- Sajili Kikundi
- Sheria za Kikundi
- Akaunti za Benki
- Kategori
- Mifuko ya Jamii

✚ Wanachama

- Tazama wanachama
- Sajili Mwanachama

✚ Fedha

- Ununuzi wa Hisa
- Mikopo na Marejesho
- Uwekaji wa Mifuko ya Jamii
- Mikopo ya Jamii na Marejesho
- Miamala / Transactions
- Mgao au Dividend
- Kujitua uanachama



✚ Kibaba Changu

- Jumla ya Kisia kilichopo
- Sahihisha Taarifa zako
- Tanzama Michango yako
- Tazama Wanachama wote
- Miamala yako na ya wengine wote
- Kuweka Matangazo
- Kupiga Kura
- Kusajili Faini/Adhabu zitokanazo na Kikundi
-

MAWASILIANO

Kwa mawasiliano juu ya Kununua na Kujifunza programu hii ya Kibaba MFS, wasiliana na Timu ya Mauzo na Mafunzo.

TIMU YA MAUZO NA WATAALAM
Kibaba MFS – Ofisi za Biba Solutions,
1/2 Ali Hassan Mwinyi Road, Namanga, KND,
Box 106176, info@kibaba.co.tz | kibaba.co.tz
Dar es Salaam, Tanzania.

Unaweza kuwa Wakala wetu

by Frank Mwasalukwa

Mtu yeyote mwenye umri wa miaka 18+ anaweza kuwa wakala wa Kibaba MFS kwa kujisali bure kwenye Tovuti ya Kibaba ambayo ni www.kibaba.co.tz kisha kuweza kusajiri vikundi mbalimbali vya ViCoBa na vingine vya aina hiyo vyenye uhitaji wa kutumia mfumo huu wa Kibaba MFS.

Miliki wa Kibaba MFS (Biba Solutions)


Miliki na mwenye haki zote juu wa Mfumo wa Kibaba MFS ni Kampuni inayojishughulisha na maswala ya IT na utengenezaji mifumo ya Kompyuta ya Biba Solutions Ltd. Kampuni hii ina haki zote juu ya mfumo huu na inahifadhi haki ya Kukubali au kukataa Mtu binafsi, Chama, Kikundi, kampuni au hata Taasisi yeyote ya (Kiserikali

na isiyo ya Kiserikali) kununua na kumiliki mfumo wa Kibaba MFS.

Kibaba MFS imesajiriwa na chama cha Haki miliki cha Tanzania (COSOTA) nembo na majina yanayotumika (Kibaba, Kibaba MFS na Kibaba Haba na Haba) yana utambulisho wa kutumika kama alama za Biashara (Trade Mark au TM) kutoka kwa Wakala wa Serikali wa Usajiri na utoaji Leseni (BRELA).

Kibaba inalindwa na Haki ya Kitaifa na Kimataifa kupitia muunganiko wa Vyama vya Haki Miliki Duniani kupitia chama cha Tanzania cha COSOTA.

Inaendelea Uk 3



Picha ya hapo juu inaonesha muonekano wa Programu ya Kibaba inavyo onekana kama utoingia kwa kutumia Kompyuta. Ingawa pia unaweza kutumia Tabiti au Simu Janja



MATUKIO MBALIMBALI



Mkutano wa Ngazi ya Juu

Mikutano ya Ngazi ya Juu hufanyika ikishirikisha wakufunzi wa ViCoBa, Wakufunzi wa ICT na wadau mbalimbali kwenye Tasnia ili kuboresha mfumo huu, ili kuja na Masasisho ya Maboresho mapya ya Kibaba ambayo hufanyika mara kwa mara



Kifaa chochote, Popote

Hivi unajua kwa uwezo wa Intanet, unaweza kutumia simu janja, Tableti au Kompyuta?, fanya hivi, fungua brauza ya kifaa utumiacho, andika demo.kibaba.co.tz kwenye sehemu ya kuandika anuani. Ikifunguka andika username: admin na Nenosiri andika 123456.

FAST FACTS

99.9%

Mkatataba wetu na Watumiaji wa Program ya Kibaba ni kuwa hewani kwa Masaa 24/7 na siku 365. Ni Intanet tuu ndo itakufanya uingie kuangalia mtiririko wa Miamala yako ya Fedha kwenye kikundi

05%

Inatumia kiasi kidogo sana cha Intaneti, yaani chini ya 5 MB utakuwa umemaliza kufanya Miamala yote ya siku.

ZAIDI KUHUSU KUJARIBU MATUMIZI

Yeyote anaweza kujaribu kutumia programu, ingia kwenye Poto yetu na ujifunze zaidi

PORTAL YA KIBABA
www.kibaba.co.tz

Uwakala....

Inaendelea

Wajibu wa Wakala kwa Mmiliki

Wakala atawajibika kuwasilisha malipo yote ya Mteja kwenye Ofisi za Kibaba MFS au Bibo Solutions Ltd au Mpesa/tiGO Pesa au Benki kabla huduma haijaanza kutolewa. Wakala hato ruhusiwa kutoza zaidi ya 10% ya bei pendekezwa, hii aihuishi Mapatato ya Wakala na Wateja wake juu ya Mafunzo ya matumizi ya Kibaba MFS.

Wakala atawajibika kuleta taarifa zote muhimu zikiwemo (Simu, email, anuani ya Posta na Eneo) za Kikundi anacho kisajiri, hii itasaidia kuvifikia vikundi ambapo Wakala atakua ameacha uwakala.

Wajibu wa Mmiliki kwa Wakala

Mmiliki wa Kibaba MFS anawajibika kutoa mafunzo na matirio (Machapisho) ya Kibaba MFS kwa Wakala alisajiliwa kwa wakati ili kumwezesha Wakala kuwahudumia wateja wake. Wakala atapata 10% ya Mauzo ya Kibaba MFS, pesa hii itakusanywa na malipo kufanyika kwenye Akounti ya wakala (Benki au Simu).

Mmiliki anawajibika kutoa huduma ya kuwepo kwa mfumo wa Kibaba MFS hewani (Online) kwa masaa 24 ndani ya wiki na mwaka (24/7365) ndani ya kipindi ambacho mteja atakuwa amelipia huduma.

Mmiliki atatoa msaada na sapoti kwa kipindi chote cha maisha ya Mfumo, hii itahusisha kuandaa na kusambaza machapisho, Msaada hewani (Online Support) na kuwezesha Mijadala hewani na kutoa Masasisho ya mara kwa mara (Updates).

Kuachana na Uwakala wa Kibaba MFS

Wakala atakuwa amejiondoa mwenyewe kuwa wakala kama atafanya yafuatayo

1. Kutofuata sheria za Nakala hii
2. Kufanya Kosa la Jinai na Mahakama kuthibisha
3. Malalamiko kutoka kwa Wateja na kujiridhisha ni malalamiko ya kweli
4. Kutifikisha michango / Ada za wateja
5. Kuamua mwenyewe kuacha
6. Kutoza Ada zaidi ya 10% ya bei Pendekezwa



Kujiunga kuwa Wakala

Kwa yeyote anaetaka kuwa wakala atajaza fomu kwenye Tovuti hii na Timu ya kibaba itamthibitisha kwa kukubali au kukataa kwa yeye kuwa **Wakala** wa Kibaba MFS.

Kwa yeyote ataka kuwa amejitoa uwakala, atatakiwa kijiunga tena kwa kujaza fomu upya ili kuwa wakala.

Mawakala wote watachapishwa kwenye Tovuti hii pindi tu watakapopitishwa na Timu ya Kibaba MFS.

Tumia kiungo hiki kusajili uwakala



UWAKALA



Taasisi za ViCoBa, Taarifa Muhimu

Kibaba Imefanya maboresho mapya ya mfumo wake wa Kibaba, na sasa kuna toleo jipya la Kibababa Toleo Na. 2.1.0. Pamoja na mabadiliko mengi, Tumeongeza kipengele kilichokuwa kinasubiriwa na Waratibu wa Wilaya na Kitaifa kuoka Taasisi mbalimbali Tanzania nzima.

Kipengele hicho kipya (New Feature) Kinaitwa Link to External Viewer au kwa kiswahili Kitambulisho cha Mwangalizi wa nje. Kipengele hiki kimebuniwa ili kuendelea kurahisisha kazi za wana ViCoBa na Waratibu wa Wilaya na Taifani.

Kwa sasa kuna Mifumo ya Aina mbili, Kibaba MFS na Kibaba Waratibu. Kwa sasa inamaana waratibu wote wa ViCoBa

watapewa mfumo wao na jina maalum la kutumia.

Faida ya Mratibu kwenye Mfumo

Mratibu akiingia kwenye mfumo huu atakuwa na uwezo wa kuona Taarifa za kikundi / Vikundi ambavyo viko chini yake. mfano, Vikundi vya wilaya ya Misungwi na Mratibu wao wamepewa numba maalumu ambayo wataitumia kuwasiliana kwa kutumia mfumo wa kibaba.

Hii itarahisisha kazi za kukusanya taarifa kwa kutumia karatasi, au ujumbe mfupi wa simu, pia itasaidia waratibu kupunguza safari za kila siku kwenda kutembelea Vikundi vya ViCoBa ili tu, kupata taarifa. Mfumo huu wa LTEV pamoja na Kurahisisha kazi, umeleta kuwa na taarifa za uhakika na kwa haraka

(Consistence and Efficiency) kwa kutumia simu zao au Kompyuta zao.

Nini cha Kufanya kama Mratibu

Ili mfumo huu wa LTEV ufanye kazi, basi waratibu lazima waongee na Vikundi vyao na kuvipatia namba hizo ili wana ViCoBa waweke kwenye mfumo wao wa Kibaba MFS. Vikundi vitatakiwa kutuma / Kukubali kuweka namba hizo za LTEV kwenye mfumo ili Waratibu wazipate taarifa zao.



Mafunzo ya Jinsi ya Kuandaa na Kutumia mfumo wa Kibaba Wilaya ya Ilala - Dar es Saam

Timu ya Kibaba imeendesha mafunzo ya jinsi ya kuandaa na kutumia mfumo wa Kibaba kwa wanachama viongozi wa Vikundi vya ViCoBa, safari hii ilishirikiana na taasisi isiyo ya kiserikali ya "Young Women Christian Association" kama inavyojulikana zaidi kwa jina la YWCA.

Mafunzo hayo yaliwalenga wanachama viongozi wa Vikundi vya VICOBBA vilivyonunua mfumo wa Kibaba kwa wilaya ya Ilala, Dar es Salaam ambavyo vinasimamiwa na taasisi ya YWCA Tanzania. Mafunzo yalilenga kuwapa uwezo wa uelewa



wa jinsi mfumo mzima wa Kibaba unavyofanya kazi, yaani kuanzia utarishaji wa mfumo, mahali data zao zitahifadhiwa, jinsi mfumo unavyofanya kazi na matumizi yake kwa ujumla.

Frank Mwasalukwa, ambaye ni kiongozi wa Mradi wa Kibaba, alianza kwa kutoa utambulisho wa mfumo na wapi wazo la kutengeneza Mfumo wa Kibaba ulipotokea,

Tuliama kutengeneza mfumo huu ili kukidhi haja ya uhitaji wa utunzaji wa taarifa za kikundi chetu binafsi cha ViCoBa – Alisema Mwasalukwa

Aliendelea kuwaeleza washiriki juu ya Mfumo wa Kibaba unavyoshirikiana na mifumo mingine duniani ili kufikisha huduma kwa uhakika na upatikanaji wa huduma hewani kwa asilimia 99.9% bila kukatika, Kibaba MFS inashirikiana na mfumo wa Microsoft

Azure kuhifadhi taarifa za wanachama wa ViCoBa wanaotumia mfumo wa Kibaba. Microsoft Azure imethibitishwa kuwa yenye Ufanisi wa hali ya juu na ya Kuaminika.

Mafunzo yalifanyika Tarehe 09 Machi 2017 yalianza saa 3 Asubuhi na kumalizika saa 10 Jioni katika ukumbi wa Taasisi ya YWCA Tawi la Dar es Salaam, Buguruni Malapa.

ASANTE KWA KUTUAMINI

Nichukue fursa hii kuwashukuru wote kutoka taasisi mbalimbali na vikundi vya ViCoBa kwa kutuamini na kutupa nafasi ya kuwahudumia, mpaka sasa tuna vikundi 250+.

Frank Mwasalukwa
Project Led



Je, Unajua Faida za ViCoBa?

by Rogers B. Fungo

Vicoba (Village Community Bank) ni mfumo wa kuweka na kukopa kwa wanachama waliojiunga kwa pamoja na kuunda kikundi kwa malengo ya kujikwamua kutoka kwenye umaskini.

Mfumo huu ulianza Tanzania miaka 10 iliyopita na umeonyesha mafanikio makubwa kwa wanachama kukopesha na kusaidiana katika matatizo mbalimbali na pia kuanzisha miradi ya kiuchumi.

Vicoba vimesaidia asilimia kubwa ya wananchi kujikwamua na umaskini ambao umetawala. Kupitia Vicoba, jamii imepanua maendeleo yake na taifa kwa ujumla.

Vicoba hutoa mafunzo ya kuongeza ujuzi wa biashara kwa wanachama kupewa fursa au kipaumbele cha kupata mafunzo na ujuzi wa biashara ili kuleta ongezeko na faida kwenye biashara wanazojihusisha nazo.

Hutoa mafunzo juu ya ujasiriamali na biashara mbalimbali. Hufundisha jinsi ya kuwa mjasiriamali na kubainisha anatakiwa aweje, nini maana yake na faida zake.

Mara nyingi huwafundisha kutengeneza bidhaa mbalimbali ikiwamo sabuni za maji, magadi na bidhaa nyinginezo.

Huwasaidia wanachama kutafuta masoko ya uhakika kwa ajili ya kusambaza na kuzaa bidhaa zao kwa bei yenye faida bila wao kunonywa.

Wanachama wanaweza kupata mitaji ya biashara kutoka kwenye kikundi ambayo itawawezesha kuanzisha au kuendeleza biashara zao. Biashara za wanachama zitaweza kukua kutoka kwenye kiwango cha chini au kutoka kwenye biashara ya mtaji mdogo mpaka kuwa mkubwa.

Ndiyo kusema si ajabu mjasiriamali aliyeanzia kwenye Vicoba akajikuta anakuwa mfanyabiashara mkubwa anayetegemewa na Taifa katika kuongeza mapato yake kupitia kodi mbalimbali.

Unaweza usiamini lakini haya yanawezekana iwapo mhusika atakuwa makini na kufuata kanuni sahihi za kibiashara zilizobuniwa vizuri.

Vicoba pia husaidia kukuza uchumi wa wanachama au wanakikundi kutokana na shughuli ambazo wamekuwa wakijihusisha nazo na ambazo zimekuwa zikiwaletaka maendeleo.

Familia ambazo zimekuwa zikijihusisha na vikundi hivi, zimekuza uchumi na kupiga hatua nzuri ya kujikimu.

Kukua huku kwa uchumi wao kumezondolea familia mizigo mingi ambayo ilikuwa ikiwakabili ikiwamo ile ya, kusomesha watoto pamoja na pesa ya matibabu pale kunapokuwa na mtu mgonjwa katika familia.

Hutoa mikopo kwa wanachama, ambayo inawasaidia wanachama (jamii) katika shughuli za kimaendeleo ikiwamo biashara.

Lakini mikopo hii ni nafuu kwa sababu inakuwa na riba ndogo kuliko mikopo ya taasisi nyingine. Riba yake haizidi asilimia 10 katika marejesho yake, hii inasaidia wanachama waweze kurejesha kwa wakati na kwa wepesi.

Wanachama wa Vicoba wana umoja ambao pindi panapotokea matatizo ikiwamo misiba na ugonjwa, husaidiana.

Endapo mwanachama mmoja au zaidi wamefikwa na msiba, kuugua au kuuguliwa, wanachama husaidiana kwa asilimia kubwa kwenye shughuli hiyo kama vile inavyokuwa kwa ndugu wa familia moja.

Pia, Vicoba vinaleta umoja na ushirikiano katika jamii. Wanachama hufanya kazi au vitu vya maendeleo kwa umoja na kwa kushirikiana wote kuanzia kwa viongozi na watu wote.

Vinadumisha upendo baina ya watu kutokana kuwa bega kwa bega katika matatizo na katika sherehe na shughuli mbalimbali.

Kutokana na utaratibu wa wanakikundi kushirikiana katika misiba, maradhi na sherehe, kitendo hicho kinawafanya kuwa karibu na kutambuana.

VICOBA INA FURSA NYINGI



Moja ya Vikao vya ViCoBa

Pia vikundi hivi vinatoa ajira kwa wanachama. Vimekuwa vikitoa ajira kwa wanachama kutokana na miradi mbalimbali ambayo wamekuwa wakianzisha kutokana na mafunzo ya biashara wanayopata.



Mfano wa Kitabu cha Hisa

Wanachama wametumia fursa hizo kama moja wapo ya sehemu ya kupata ajira na kujikwamua kiuchumi. Hii siyo kwa wasio na ajira tu, bali hata wale walioajiriwa, lakini kipato chao ni kidogo.



ViCoBa ni kwa yeyote

Vicoba vimesaidia asilimia kubwa ya wananchi kujikwamua na umaskini ambao umetawala. Kupitia Vicoba, jamii imepanua maendeleo yake na taifa kwa ujumla.

ViCoBa na Changamoto za Utunzaji wa Data

Vicoba ni mfumo wa kuweka na kukopa kwa wanachama waliojiunga kwa pamoja na kuunda kikundi kwa malengo ya kujikwamua kutoka kwenye umaskini.

Mifumo ya Uendeshaji

Mfumo wa uendeshaji wa kikundi cha ViCoBa hutofautiana katika sheria na utaratibu kulingana na matakwa ya wanachama. Kikundi cha ViCoBa kinakuwa na Wanachama wasiozidi 30, Kikundi kinajiweka utaratibu wa siku ya kukutana kwa nafasi zao, pia kikundi huweka kiasi cha thamani ya Hisa moja na idadi ya hisa zisizozidi 5 kwa mwanachama ambazo zita nunuliwa mara moja kila wakutanapo.

Utungaji wa Sheria binafsi na Nidhamu ya Pesa

Kikundi kinaweza kuweka utaratibu wa michango kadri wanavyoona inafaa kwa ajiri ya maendeleo ya Kikundi na wao wenyewe Binafsi. Kwa mfano kikundi kinaweza kuweka kiasi cha adhabu kwa wachelewaji kikaoni au adhabu kwa wasiohuhuria vikao, wanaweza kuongeza mifuko mingine ya Jamii kadri wanavyo hitaji.

Ki msingi, Mfumo wa ViCoBa hutumia Kadi za kurekodi Hisa na Mapato ya Kikundi/ wanachama na Sanduku hutumika kama kifaa cha kuhifadhi Pesa na nyaraka mbalimbali za Kikundi zikiwemo kadi za kutunza Taarifa.

kulingani na ukuaji wa vikundi vya ViCoBa na changamoto za utunzaji wa Fedha na Taarifa zake umekuwa ni shida sana, wakati mwingine, taarifa za wanachama hupotea kuokana na sababu mbalimbali kama majanga yasiyotarajiwa ya Wizi, Mafuriko na mengineyo. Vikundi vikiwa na pesa za nyingi huamua kufungua akaunti ya Fedha benki au kwenye akaunti za simu za mkononi, lakini Taarifa za wanachama hubaki kutokuwa salama kwa kutotunzwa vizuri.

Kibaba MFS ni mfumo wa kurahisisha kazi za ViCoBa ili kuleta ufanisi kwenye utunzaji wa Taarifa binafsi za wanachama na taarifa za Fedha. Kwa kutumia kibaba utaweza kuepukana na ujazaji wa taarifa zako kwenye Vitabu na kadi zisizo salama au matumizi ya Spreadsheet (Excel).

Mfumo wa Kibaba MFS, humuezesha mweka hazina wa kikundi kupata taarifa za fedha za mwanachama yeyote, wakati wowote kwa kutumia kifaa chenye uwezo wa wavuti (Internet). Vifaa kama Simu Janja (Smart Phone), Tablet na Computer vikiwa na internet basi atapata huduma hiyo.



Kibaba – Programu ya ViCoBa

1/2 Ali Hassan Mwinyi Road, mkabala na
Don Bosco VTC – Oyster bay, Box 106176
Namanga, Msasani – KND, Dar es Salaam, Tz
Simu: 0713 302 950 | 022 2664 739
Pepe: info@kibaba.co.tz | www.kibaba.co.tz